BWANA MWANIKI

# MATBAA YA TARGETER

# UBASHIRI WA KWANZA WA KCPE MWAKA - 2021

## DARASA LA NANE

**STAHIKI 007**

## KISWAHILI:
## SEHEMU YA KWANZA:
## LUGHA

**Muda: Saa 1 Dakika 40.**

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA**
**SOMA MAAGIZO YAFUATAYO KWA MAKINI .**

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibu. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu, andika katika kijitabu hiki.
3. Ukiisha kuchagua jibu lako, lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala sio katika kijitabu cha maswali.

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU.**

4. Tumia penseli ya kawaida.
5. Hakikisha ya kwamba umeandika yafuatayo katika karatasi ya majibu.

**NAMBARI YAKO YA MTIHANI**
**JINA LAKO**
**JINA LA SHULE YAKO**

6. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani nambari ya shule, na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu, na usiikunje.
9. Kwa kila swali **1-50,** umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi **A, B, C, D.** Ni jibu **MOJA** tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

**Mfano**

**Katika kijitabu cha maswali: Jibu maswali kulingana na maagizo uliyopewa.**

**18.** Jumla ya miaka mia moja huitwa _______________

A. mwongo mmoja  B. alfeni
C. Karne  D. Kikwi moja

Jibu sahihi ni **C**

Katika karatasi ya majibu

**16.** [A] [B] [C] [D]  **17.** [A] [B] [C] [D]  **18.** [A] [B] [~~C~~] [D]  **19.** [A] [B] [C] [D]

18, kisanduku chenye herufi **C** ndicho kilichochorwa kistari.

11. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
12. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku **kimoja** tu kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

**Kijitabu hiki cha maswali kina kurasa 8 zilizopigwa chapa.**

**GEUZA UKURASA**

*Huchapishwa na kuratibiwa na taasisi ya uchapishaji ya Targeter Educational Publishers Ltd.*
*Email: info@targeterpublishers.co.ke*

UBASHIRI WA KWANZA WA KCPE 2021

Scanned by CamScanner

***Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.***

Taifa __1__ la Kenya shughuli __2__ zimekwama. Ugonjwa wa Covid-19 umetetemesha kila kona ya taifa__3__. Ni vizuri kuelewa kuwa, gonjwa hili __4__ nchi yetu tu __5__ pia ulimwengu mzima. Hata mataifa yenye uwezo mkubwa kiteknolojia, kiuchumi na elimu ya juu __6__ adha ya ugonjwa huu tandavu wa Covid-19. Ili kujikinga, yafaa tunawe mikono __7__ sabuni, kutoshiriki mikutano na ikiwezekana tufanye kazi __8__ nyumbani.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | **A.** nzima | **B.** zima | **C.** mzima | **D.** lizima |
| **2.** | **A.** zote | **B.** yote | **C.** lote | **D.** vyote |
| **3.** | **A.** yetu | **B.** zetu | **C.** wetu | **D.** letu |
| **4.** | **A.** limetisha | **B.** umetisha | **C.** halijatisha | **D.** litatisha |
| **5.** | **A.** bali | **B.** hata | **C.** kumbe | **D.** ikiwa |
| **6.** | **A.** haijaepuka | **B.** hayajaepuka | **C.** haujaepuka | **D.** halijaepuka |
| **7.** | **A.** ya | **B.** na | **C.** kwa | **D.** za |
| **8.** | **A.** katika | **B.** kwa | **C.** kwenye | **D.** kutoka |

Waswahili walisema __9__. Hali hii ilijitokeza pale Kadongo aliyekuwa na mali __10__ alipoamua __11__ masomo ya yatima mmoja. Uamuzi wake huo uliwashangaza wengi kuona matajiri wengi __12__ kusaidia __13__ kuwa wamiliki wa mali yafuatayo __14__ majumba, magari, mashamba na viwanda. Ni vyema kuwa na __15__ kama Kadongo.

**9.** **A.** hiari yashinda utumwa  **B.** mtu hujikuna ajipatapo
**C.** kutoa ni moyo usambe ni utajiri  **D.** mwenye shibe hamjui mwenye njaa

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **10.** | **A.** madogo | **B.** ndogo | **C.** nyingi | **D.** kidogo |
| **11.** | **A.** kuyathamini | **B.** kuthamini | **C.** kuyadhamini | **D.** kuidhamini |
| **12.** | **A.** walidinda | **B.** walikubali | **C.** waliamini | **D.** waliamua |
| **13.** | **A.** sembuse | **B.** ili | **C.** licha ya | **D.** kabla ya |
| **14.** | **A.** ; | **B.** : | **C.** _ | **D.** ! |
| **15.** | **A.** mkono mzito | **B.** mkono wa birika | **C.** mkono wa buli | **D.** mkono wazi |



Scanned by CamScanner

***Kutoka swali la 16 mpaka 30, chagua jibu lililo sahihi.***

16. Katika neno, '**alisahaulika**' tambua kiambishi kiwakilishi cha nafsi na cha wakati.

A. A, ka

B. li, li

C. li, ka

D. A, li

17. ***Andika katika wingi:***

Chuma kilichovunjika kiliwekwa nyuma ya pazia.

A. Vyuma vilivyovunjika viliwekwa nyuma ya mapazia.

B. Chuma zilizovunjika ziliwekwa nyuma ya pazia.

C. Vyuma vilivyovunjika viliwekwa nyuma ya pazia.

D. Machuma yaliyovunjika yaliwekwa nyuma ya mapazia.

18. ***Andika katika udogo:***

Mzee alipiga ngoma kwenye mji.

A. Zee lilipiga goma kwenye jiji.

B. Vizee vilipiga vigoma kwenye vijiji.

C. Kizee kilipiga kigoma kwenye kijiji.

D. Mzee alipiga kigoma kwenye jiji.

19. ***Tegua kitendawili kifuatacho:***

Kikigongwagongwa wanawe hutoka.

A. Kizimba

B. Kichuguu

C. Mzinga

D. Chungu

20. Chagua sentensi yenye kivumishi cha pekee.

A. Gari lolote lililoendeshwa pasipofaa litaondolewa.

B. Ndugu yangu atasafiri kesho.

C. Ndizi mbovu zimeliwa na ng'ombe.

D. Kabati hilo ndilo lililotengenezwa.

21. Chagua methali yenye maana kuwa mtu anaposababisha shida huishia kuwahusisha jamaa wake.

A. Mla nawe hafi nawe ila mzaliwa nawe.

B. Mchumia juani hulia kivulini.

C. Kikulacho ki nguoni mwako.

D. Mchuma janga hula na wa kwao.

22. ***Kanusha sentensi ifuatayo:***

Kujitahidi kwangu kuna manufaa.

A. Kujitahidi kwangu hakuna manufaa.

B. Kutojitahidi kwangu hakuna manufaa.

C. Kujitahidi kwangu hakutakuwa na manufaa.

D. Kutojitahidi kwangu hakutakuwa na manufaa.



Scanned by CamScanner

RWANA MUCHIRI

**23.** Jina **"shughulika"** lina silabi ngapi?

A. 10

B. 8

C. 4

D. 6

**24.** 'Cherahani' ni jina katika ngeli gani?

A. KI - VI

B. I - ZI

C. U - ZI

D. LI - YA

**25.** Ni kiungo kipi cha mwili kinachosafisha hewa?

A. Ini

B. Wengu

C. Figo

D. Pafu

**26.** ***Unganisha sentensi ifuatayo:***

Mama alipika wali. Wali ulikuwa kwa Leah.

A. Wali ulipikiwa kwa Leah na mama

B. Mama alipikiwa wali kwa Leah

C. Leah alipikiwa wali kwa mama.

D. Wali ulipikwa na Leah kwa mama.

**27.** ***Tambua maneno yaliyopigiwa kistari:***

Vitabu vizuri vitanunuliwa kesho.

A. Kielezi, nomino

B. Kivumishi, nomino

C. Kivumishi, kielezi

D. Kielezi, kiwakilishi

**28.** ***Andika katika usemi wa taarifa:***

"Tutapiga kambi hapa kesho," wanajeshi walisema.

A. Wanajeshi walisema watapiga kambi hapo kesho.

B. Wanajeshi walisema walipiga kambi hapo kesho.

C. Wanajeshi walisema kuwa wangepiga kambi hapo baadaye.

D. Wanajeshi walisema kuwa wangepiga kambi hapo siku ambayo ingefuata.

**29.** Mkopo usiotozwa riba huitwaje?

A. Arbuni

B. Chirimiri

C. Kadhongo

D. Karadha

**30.** ***Andika kwa tarakimu:***

Milioni sita, mia tisa tisini na tisa elfu, mia tisa tisini na nane.

A. 6,996,998

B. 6,999,988

C. 6,999,998

D. 6,909,098



Scanned by CamScanner

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 mpaka 40.***

Aghalabu kila wakati nilipomtembelea nyanya yangu, a'ikuva akinitambia hadithi. Basi nilipomtembelea mwezi Juni, aliweza kunitambia hadithi kuhusu Mzee Hekima na bibi yake. Waliishi katika kijiji cha Madongo. Mzee Hekima alijaliwa na Mola na watoto wengi wavuli kwa magashi. Nao waliwalea wanao vyema kwa kuwalisha vizuri vyakula vya tumboni na kiroho. Usisahau kuwa Mzee Hekima alikuwa tajiri wa mali na moyo. Mamia ya wanakijiji waliofika kwake kumlilia hali aliwasubilia kwa vyote. Kuna wale waliopewa riziki kwa kulima shambani, wengine kufagia boma lake bora tu kila mmoja alifaidika na mkono karimu wa bwana huyu.

Kati ya watoto wake wengi, Mzee Hekima alimpenda zaidi kitindamimba na alimpendelea kwa mengi. Kutokana na hali hii kitindamimba alianza kujivuna na kuwadharau wakubwa wake. Alionyesha kiburi, unyeti na dharau. Mwishoni tabia yake ilianza kuingia ufa. Mambo yalizidi kuzorota zaidi kiasi cha mtoto huyo kuwa mbaya zaidi. Wazazi walipogundua uovu wa mtoto huyo, mambo yalikuwa yamekwisha kithiri. Baada ya kujaribu kulihali kumwongoa na kulemewa walimtupa jongoo na mti wake.

Kila mmoja aliepuka kitinda mimba huyu kama kinyamkera. Hakushirikishwa michezoni wala katika matembezi. Ajabu ni kwamba, hakurekebisha tabia yake bali aliendelea kuwa mkaidi zaidi kuliko hata mkia wa nguruwe. Mzee Hekima naye alizidi kuzeeka na kudhoofika kadiri siku zilivyosonga.

Mzee Hekima alianza kuwausia wanawe. Aliweka kila kitu wazi. Alisema pesa zote za banki zingegawanywa kwa wanawe wote wa kiume. Nayo mali yaliyobaki yagawanywe kulingana na umri wa kila mrithi. Jukumu la uandishi wa wosia huu lilipewa kitindamimba. Naye akawa amepata nafasi murua ya kufanya hila. Alijiandikia nafasi kubwa ya urithi wa mali ya baba yake. Basi Mzee Hekima alipoaga dunia yule kitindamimba aliazimia kuuza shamba lile Hapo alimtafuta mnunuzi na kumpata Mzee Johara. Walipatana bei lakini hakulipwa pesa taslimu ila waliandikiana mkataba.

Nakumbuka siku moja, mtoto wa Mzee Johara alienda mtoni kuogelea akiwa ameandamana na marafiki zake. Mto Kingo ulijulikana kwa kuwa na mamba wengi waliowashambulia wakazi wa eneo hilo. Kwa bahati mui mwanawe Mzee Johara alishikwa mguuni na mamba. Alivutwa na kuelekezwa kwenye maji makuu. Watoto wenzake walipoona hivyo walipiga usiahi kwa hofu wakiomba msaada. Kwa bahati nzuri, wana wawili wa yule Mzee Hekima walikuwa wakipita njia karibu na mto huo. Wakasikia mayowe na kelele. Basi bila kulimatia wakaenda haraka kuangalia kelele zilikuwa za nini

Baada ya kufika mtoni, waliambiwa habari za mtoto yule aliyechukuliwa na mamba. Walipotupa macho walimwona mtoto yule wa Mzee Johara akizamia lulu majini. Bila chelewa chelewa, vijana hawa walivua nguo zao na wakajitosa majini na kumfuata mamba yule Walishambulia mamba yule kwa sime zao mpaka akamwachilia mtoto yule Wakamchukua na kuogelea naye hadi ufuoni ya mto. Hapo walimpa ganga ganga za mganga zinazomwacha mgonjwa na matumaini.

Mtoto huyo alikuwa amejeruhiwa vibaya mguuni kutokana na kuumwa kwa meno ya mamba. Baada ya kumpa huduma ya kwanza waliamua kumpeleka kwa baba yake ili kumsimulia kisa chote. Mzee Johara alifurahishwa sana na kitendo cha watoto hao na akawaombea dua ya Mola awasaidie.

Baada ya kuwapa makaribisho aliamua kuwasindikiza wana wale wawili huku yeye akielekea kumlipa kitindamimba pesa zake. Basi wote watatu waliondoka. Wana wale walienda nyumbani naye Mzee Johara akielekea kumlipa ujira wake kitindamimba. Mzee Johara aliwaomba kwa unyenyekevu waandamane naye ~~ili~~ wawe mashahidi wake. Vijana wale wawili walikubali bila ya wao kujua ni shamba gani lililokuwa likiuzwa.

Mzee Johara na ndugu wale wawili walipofika kwa mwenyeji wake, alianza kuwaelezea jinsi walivyopatana bei ya shamba. Ndugu wale wawili walishtuka sana na kukasirika. Papo hapo wakamweleza Mzee Johara kisa chote kuanzia mwanzo hadi mwisho. Mzee Johara kusikia hivyo alighairi kununua shamba hilo. Ujanja wa kitindamimba ukaponga mwamba.

31. Chagua kauli isiyo ya kweli kulingana na aya ya kwanza.
   A. Mzee Hekima na mkewe walijaliwa watoto wa kike na kiume.
   B. Mzee Hekima na familia yake walikuwa wacha Mungu.
   C. Wavulana walikuwa wengi kuliko wasichana.
   D. Mzee Hekima aliweza kutoa mwongozo mzuri wa familia yake.

32. Mzee Hekima alikuwa tajiri wa moyo kwa kuwa
   A. Mamia ya wakazi walifika kwake kumlilia hali.
   B. Alikuwa na mashamba makubwa yaliyohitaji usaidizi wa wanakijiji.
   C. Nyumbani kwake kulishiba watu walioenda kwake ili kufagia na wengine kulima.
   D. Aliwafaa wengi ambao hawakujiweza kiuchumi.

33. <u>Wazazi walipogundua uovu wa mtoto huyo, mambo yalikuwa yamekwisha kithiri.</u>Ni methali gani inayokubaliana na kauli hii?
   A. Chelewa chelewa utampata mwana si wako.
   B. Asiyesikia la mkuu huvunjika guu.
   C. Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo.
   D. Mwana wa nyoka ni nyoka.

34. Kitindamimba aliharibika
   A. kwa kuwa yeye ndiye alikuwa mtoto wa mwisho kuzaliwa.
   B. kwa kupendelewa na baba yake kuliko watoto wale wengine.
   C. kwa kupewa majukumu mengi yakiwemo yale ya ugavi wa shamba.
   D. kutokana na vijana wa hirimu yake.

35. Zifuatazo ni sifa za Mzee Hekima kulingana na aya ya **nne** ila
   A. alikuwa mwenye busara.
   B. alikuwa mwenye ubaguzi.
   C. alikuwa mwenye uwazi.
   D. alikuwa mwenye fitina.

36. Kitinda mimba kulingana na kifungu, alifaa
   A. kupata sehemu ndogo kabisa miongoni mwa warithi.
   B. kupata sehemu kubwa kabisa miongoni mwa warithi.
   C. kuliuza shamba lake baada ya kugawiwa.
   D. Kumtafuta mnunuzi wa shamba lao bila kuwahusisha ndugu zake.

37. Ujasiri wa ndugu zake kitindamimba unaonekana pale
   A. walipompeleka ndugu yao kortini kwa njama ya kuliuza shamba lao.
   B. walipoandamana na Mzee Johara hadi kwao kushuhudia ununuzi na uuzaji wa shamba lao.
   C. walipokabiliana na mamba na kumwokoa mtoto wa Mzee Johara.
   D. walipomkataza Mzee Johara kulinunua shamba lao bila idhini ya wote.

38. Ni sadfa kuwa
   A. Mzee Johara aliwaomba wanawe Mzee Hekima kushuhudia ununuzi wa shamba lao.
   B. marafiki wa mwanawe Mzee Johara hawakujua kuogelea.
   C. wana wa Mzee Hekima hawakuwahi kuacha sime kila walipotembea.
   D. kitindamimba hakuwa amelipwa pesa na badala yake waliandikiana mkataba.

39. Ni msemo gani unaoonyesha Mzee Hekima alichoshwa na kitindamimba?
   A. Mzee Hekima alimpendelea kitindamimba kuliko wote.
   B. Mzee Hekima alimpa dhima ya kuandika wosia.
   C. Mzee Hekima aliamua kugawa mali yake kulingana na umri wa kila mrithi.
   D. Mzee Hekima aliamua kumtupa jongoo na mti wake.

40. <u>Sime</u> ni
   A. upanga wenye makali kuwili.
   B. kiboko chenye ncha ya chuma.
   C. miundi inayotumiwa kulimia.
   D. ni bastola ya kufyatua risasi.



Scanned by CamScanner

*Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali 41 mpaka 50.*

Maisha ya binadamu huimarika kutokana na urafiki. Urafiki hufanya watu wanaopendana kuwa na mvuto fulani ambao huwapa kiu ya kutaka kuonana mara kwa mara. Umbali kwao huwa si chochote si lolote. Watafanya juu chini ili waweze kuwasiliana hata kama ni kwa kupigiana simu, kuandikiana nyaraka au hata kutembea kilomita nyingi mradi tu wakutane.

Manufaa ya urafiki ni gani? Nia kuu ya urafiki ni kuondoleana ukiwa, kuliwazana, kubadilishana fikira na kusaidiana wakati wa shida. Pasi na urafiki duniani kungejaa madhila, uhasama, zahama na maovu mengine ya kukiriha moyo.

Urafiki bora ni ule wa kujuliana hali, kufaana wakati wa dhiki, urafiki wa kupigiwa mfano yaani ule wa kufa kuzikana. Hata hivyo urafiki huu umeadimika kama milango ya pikipiki. Ni nadra na adimu kumpata rafiki shakiki. Kila mtu sasa ameanza tu kuamba ngoma akivuta kwake. Ya mwenzake hayamghasi, ni kanda la usufi ati.

Kile ninachojaribu kusema ni kuwa, urafiki mwingi ni ule wa juu juu. Ule wa nipe nikupe. Iwapo wewe ni maskini, ole wako! Watakwambia kuwa mkono mtupu haurambwi na utapewa kisogo. Ukiwa tajiri pia huna bahati. Utaandamwa kama nzi na kugandwa kama kupe na wanaotaka kukutia mrija. Siku ya kuonyeshwa mlango kazini watakuhepa labda uauniwe na ndugu yako.

Kulonga mithaki urafiki mwingi ni ule wa ndumakuwili. Ni ule wa kulana kivuli. Wale wanaojitapa hadharani kuwa marafiki zako shakiki ukiwapa siri, kesho utazisikia barazani. Ulimthamini lakini yeye hafai ni mfano wa kikulacho ki nguoni mwako. Ni makauleni wakubwa. Ni vyema kila mmoja ajue kuwa, ule urafiki wa zamani wa kufaana kwa jua na la mvua umezikwa katika kaburi la liliwala.

Kinyume na vile watu wengi wanavyodhania urafiki unahitaji uvumilivu, uaminifu, ukarimu, upendo, usamehevu na <u>kujitolea mhanga kama kuku ahatarishaye maisha yake ili kumwokoa kifaranga.</u>

Je, urafiki una faida? Ndiyo. Kumbuka ukiwa na marafiki huwezi kuteseka sana. Wahenga walisema kuwa mtu ni watu na hakuna mtu anayeweza kujitosheleza. Majanga yapo. Mengine makubwa yanayozidi uwezo wa mtu binafsi. Chukulia kwa mfano shughuli za mazishi. Utachimbaje kaburi na ubebe jeneza peke yako. Hapo ndipo utahitaji marafiki.

Tujue kuwa tuko pia na urafiki wa kuharibiana tabia. Kwa mfano watu wasio na msimamo kimaisha kazi yao ni kufuata wengine kama bendera. Tumewaona wengi wakijitoa kikaangoni na kujiingiza motoni bila kujali. Hawa sana sana ni wale ambao huwa hawaambiliki wala hawasemezeki. Hata wakiambiwa wasitembee na watu waovu kwa kuwa samaki mmoja akioza na mtungo pia huwa hawasikii. Huonyesha kiburi na unyeti mwishowe huishia <u>kujipalia makaa</u>.

Tamu ikizidi sana huwa sumu. Nao urafiki ukizidi sana wakati mwingi huwa na madhara yake. Unajikuta kwa kuwa ati mtu ni rafiki yako, unaamua kuchukua hatua bila hata kumhusisha. Kumbe uamuzi uliochukua ni sumu kwake.



Scanned by CamScanner

**41.** Ni wazi kuwa

A. kama si urafiki watu hawangekuwa wakionana

B. pesa haziwezi kuwa kizingiti kwa watu ambao wanataka kuonana.

C. urafiki huumua maisha ya binadamu.

D. urafiki umeanza juzi wakati wa teknolojia mpya.

**42.** Lipi si lengo la urafiki?

A. Kufarijiana.

B. Kubadilishana mawazo.

C. Kufaana wakati wa dhiki.

D. Kukirihisha moyo.

**43.** Aya ya tatu inaonyesha kuwa

A. hakuna urafiki wa kweli kokote duniani.

B. marafiki wengi ni wanafiki.

C. lengo la urafiki wowote ni kudhuriana.

D. mzigo wa mwenzio ni kanda la usufi.

**44.** Chagua methali mwafaka inayolenga mwisho wa aya ya nne.

A. Mla nawe hafi nawe ila mzaliwa nawe.

B. Akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki.

C. Nzi kufa juu ya kidonda si hasara.

D. Ndugu ni kufaana si kufanana.

**45.** Yaonekana kuwa

A. urafiki wa leo ni bora kuliko ule wa zamani.

B. urafiki wa zamani ulikuwa bora kuliko wa leo.

C. urafiki wa leo umeathiriwa pakubwa na urafiki wa zamani.

D. hakuna tofauti ya urafiki wa zamani na ule wa leo.

**46.** Taja tamathali mbili zinazojitokeza katika kauli hii:

Kujitolea mhanga kama kuku ahatarishaye maisha yake ili kumwokoa kifaranga.

A. Chuku, tashbihi

B. Tashhisi, kinaya

C. Nahau, istiara

D. Nahau, tashbihi

**47.** Mwandishi ametumia mfano wa mazishi

A. ili kuonyesha hatima ya kila mtu ni mauti.

B. kwa kuwa ni sherehe ambazo huleta majonzi katika jamii.

C. kuonyesha kuwa kuna haja ya kusaidiana wakati wa shida.

D. kuonyesha ubora na thamani ya urafiki.

**48.** Aya ya inatuonyesha kuwa,

A. kuna watu wanaotumia urafiki kwa manufaa yao ya kiuchumi,

B. urafiki wa dhati upo na unafaa kuigwa na wote.

C. wengi wa marafiki tulio nao wametufaidi sana katika shughuli zetu za kila siku,

D. hakuna msingi wa urafiki mwema.

**49.** Kujipalia makaa ina maana ya

A. kujinufaisha wao pekee

B. kujiletea matatizo.

C. kujisalimisha kwa kushindwa.

D. kukosana na watu wote.

**50.** Aya ya mwisho inaonyeshe kuwa

A. jambo zuri linaweza kuleta athari mbaya.

B. rafiki ana uwezo wa kujua shida ya mwenza.

C. hatufai kuwa na marafiki wasiojua hisia zetu.

D. ni vigumu sana rafiki kujua yale yanayomsumbua mwenzake.



Scanned by CamScanner